

# Kanuni za Maadili ya Biashara

**Corporate Compliance Office**

**+1 919 379 4300**

**Compliance@aointl.com**

Alliance One International, Inc.
8001 Aerial Center Parkway
S.L.P 2009
Morrisville, NC 27560
United States
www.aointl.com

**Version 3**
**Revised August 11, 2016**

**Kanuni za Maadili ya Biashara**


Alliance One International, Inc.

8001 Aerial Center Parkway

S. L. P 2009

Morrisville, NC 27560

Simu: +1 919 379 4300

Faksi: +1 919 379 4132




**Simu ya bure ya Msaada***

Tanzania

Piga simu kwenye namba: 704 5528215

**Tovuti:** www.aoicompliancehelpline.alertline.com

**Simu ya msaada wa uzingatiaji inaendeshwa na mtu huru wa tatu*

# Maelezo ya Uadilifu

Alliance One International, Inc. iliundwa kushughulikia changamoto za mazingira ya biashara za karne ya 21 na tumejizatiti kukabiliana na changamoto hizo kwa mafanikio katika namna zote.  Kubwa kuliko yote ni dhamira yetu ya kuendesha biashara yetu kwauadilifu kikamilifu.

Sifa yetu ulimwenguni ya uaminifu na maadili ya kutegemewa ya biashara, imejengwa na watu wengi kwa miaka mingi, itajaribiwa na kuthibitishwa katika kila biashara tunayofanya. Tuko zaidi ulimwenguni, na wenye nguvu na kumjali mteja zaidi ya ilivyokuwa mwanzo.  Lakini kiu yetu ya ubora wa ushindani na utoshelevu wa mteja huanzia na kuishia kwa kujitoa kwetu kwenye mwenendo mwemana unaozingatia sheria na kama kampuni ya kiulimwengu lazima tutengeneze na kufuatilia sheria za ulimwengu.

Kanuni zetu za Maadili ya Biashara ni mwongozo wetu katika kufuata sheria na maadili. Inaelezea wazi matarajio ya Kampuni kwa ajili ya tabia za kisheria na maadili kwa kila mwajiriwa – hilo ni wajibu, hakika, sharti la ajira. Wakurugenzi wa AOI, maafisa, waajiriwa na mawakala wanatarajiwa kuendesha biashara ya Kampuni kwa mujibu wa Kiwango kikubwa cha maadili ya kitaalam, uadilifu na uhalali wa fedha.

Sisi sote tuna mambo yetu mengi yanayohitaji muda, lakini taarifa zilizomo kwenye CBC hii zitakuwa na nguvu iwapo tutachukua muda na kufanya jitihada kusoma yaliyomo na kutumia viwango vya maadili katika shughuli zako za biashara. Kama kuna mtazamo wowote wa CBC ambao hujauelewa au kama una maswali kuhusu hali unayokabiliana nayo, hoja zako zinaweza kujadiliwa moja kwa moja na msimamizi wako, mwakilishi wa rasilimali watu, Mkurugenzi za Uzingatiaji wa Shirika. Unaweza pia kupata simu ya msaada ya masuala ya Uadilifu ya Alliance One kutoka katika maeneo yetu ulimwenguni kupitia namba ya simu bila malipo au tovuti.

Wazo lolote ambalo mafunzo ya uzingatiaji na tabia njema ya biashara kuwa halichangii chochote kwenye “la msingi”mafanikio yetu  si sahihi.  Kama AOI, kupitia utendaji wa wakurugenzi wake, maafisa, waajiriwa na mawakala ulimwenguni kote, ungeshindwa kuafikia au kuzidisha kiwango cha maadili kilichoelezewa kwenye mwongozo huu, kushindwa huko kungeweza kuhatarisha Kampuni kiuchumi, kudhuru mmoja mmoja na kuharibu moja ya vitu vya thamani vya AOI na sifa yake.  Kudumisha vitu hivi vya thamani kubwa vya shirika ni jambo la muhimu sana kwa ajili ya kuendelea kufanikiwa kwetu na uwajibikaji ambao wote tunashiriki.

Mbele yetu bila shaka italeta mazingira ya kiushindani hata zaidi na lazima tuwe tayari kukabiliana na changamoto zake; lakini lazima tujiandae kufanya hivyo bila kupunguza viwango vya maadili ambayo ni msingi wa namna tunavyoendesha biashara yetu.



# Yaliyomo

## Utangulizi


Kuhusu Sera yetu ........ 1

Sheria gani inatumika ........ 2

Misamaha ........ 2

Alliance One International na Wewe ........ 2

Kutolipiza Kisasi ........ 3

Simu ya Msaada ya Masuala ya Uzingatiaji ........ 3


## Kufanyia Kampuni Yetu Kazi

## Sera


Ufaragha wa Binafsi ........ 4

Migogoro ya Kimaslahi ........ 5

Uuzaji wa Hifadhi ........ 5

Fursa za Shirika ........ 7

Hongo na Rushwa ........ 7

Utoaji Zawadi, Safari na Burudani kwa Maafisa wa Serikali ........ 11

Shughuli za Kisiasa na Michango ........ 13

Kupokea/Kutoa Zawadi kwa Wateja Binafsi na Wasambazaji ........ 13

Michango ya misaada na Ufadhili wa Shirika ........ 14

Utumizi wa Mawakala Wengine ........ 14

Nje ya Ajira, Maslahi na Uwekezaji wa Bishara ........ 14

Matumizi ya Programu za Kompyuta ........ 15

Usiri ........ 15




Taarifa Sahihi ya Fedha ........................................................................ 16

Mawasiliano kwa Umma ........................................................................ 16

Fidia na Mafao ........................................................................ 17

Kutokuwa na ubaguzi, Fursa Sawa na Kutobughudhiwa .......................... 17

Ushirikiano katika Kuchunguza Makosa .................................................. 18

Udhibiti wa Kumbukumbu ........................................................................ 18

## Kufanya kazi kwenye mazingira Yetu

Mahali pa Kazi pasipo na Dawa za Kulevya............................................ 19

Afya na Usalama ........................................................................ 19

Ajira kwa Watoto, Ajira ya Lazima na Haki Nyingine za Binadamu............20

Sheria za Mazingira ........................................................................ 20

## Kufanya kazi Kwenye eneo la Soko

Kupinga Mgomo ........................................................................ 20

Sheria za Shirikisho za Makosa ya Jinai kuhusu Udanganyifu.................... 21

Uwajibikaji wa Raia ........................................................................ 21

Ubadhirifu wa Fedha ........................................................................ 21

Kupinga Dhamana na Ushindani Uliosawa ............................................. 22

Vikwazo vya Biashara ........................................................................ 25

Sheria za Usafirishaji na Forodha ........................................................... 25

## Hitimisho & Muhtasari

Muhtasari wa Sera Yetu ........................................................................ 27



# Kuhusu Sera yetu



Moja ya maadili yetu katika AOI ni kujitoa kwetu kwa uadilifu. Namna tunavyofanya biashara na namna tunavyowahudumia wengine itaitambulisha Kampuni ulimwenguni kote. Ni muhimu kwa wahisa wetu, wateja na wasambazaji wetu, kwa waajiriwa wetu wote duniani kote na kwa jamii ambako tunaishi na kufanyakazi kwamba AOI inajulikana kwa uadilifu wa watu wake na viwango vyake vya hali ya juu vya maadili ya biashara.

Tabia za kimaadili zinaweza kuwa na maana zaidi ya kuzingatia sheria – lakini huanza na sheria. Unawajibika kukubali kupata maarifa ya kutosha kuhusu sheria zinazohusiana na mahali ulipo na majukumu na kazi zako mahususi ili kubaini mwenendo au hali ambayo inaibua maswali ya kisheria au maadili na wakati gani wa kutafuta ushauri wa kisheria. Ni wajibu wa uongozi kuhakikisha na kuwezesha kutii kiwango kikubwa cha maadili kwa kuwasilisha kwa uwazi mahitaji ya CBC na kusaidia utumikaji wake wa haki kwa wafanyakazi wote.

Lengo la CBC ni kutoa muhtasari wa sera ya Kampuni kwa ujumla na kutoa mwongozo kwa ajili ya mwenendo mzuri katika maeneo ya masuala mahususi. Inaelezea matarajio ya kimsingi ya Kampuni kuhusiana na na tabia yako ya kitaalam na kibinafsi. CBC haifafanui kila mwenendo ambao haukubaliki au uko kinyume na sheria. Kwa sababu mwenendo fulani haukujadiliwa hii haimaanishi kwamba kitendo kinakubalika na/au kinaruhusiwa. Kampuni inatarajia kila mkurugenzi, afisa, mwajiriwa na wakala duniani kote kufanya juhudi nzuri kuelewa na kukubaliana na barua kwa vyovyote vile katika sera za AOI na sheria zinazotumika. Ufuatiliaji wa matarajio haya kila mkurugenzi, afisa, mwajiriwa na wakala anahitajika kuthibitisha kwamba atakubaliana na CBC.

Wakati ukiukaji unaodaiwa wa CBC unaporipotiwa, Kampuni itachukua hatua ya haraka na inayofaa kwa mujibu wa sheria inayotumika na desturi njema za biashara. Kukosa kutii viwango vilivyowekwa na CBC kunaweka wewe, wafanyakazi wenzako, na Kampuni kwenye hatari, na kunaweza kukufanya kuchukuliwa hatua ya nidhamu pamoja na upigwaji kalamu. Katika hali fulani, kukosa kutii CBC hii kunaweza pia kusababisha kupeleka suala hili kwenye mamlaka ya serikali yanayofaa.

Haiwezekani kushughulikia kila hali unayoweza kukabiliana nayo. Mwishowe, lazima tusaidiane kwenye msimamo wetu kufanya biashara kwa njia sahihi na tunapokuwa hatuna uhakika juu ya sababu sahihi ya kitendo tunapaswa kutafuta ushauri kwa wenzetu na washauri. Kwa baadhi ya mambo, hali inaweza kuwa ngumu ambayo mwongozo wa ziada unahitajika. Mkurugenzi wa Uzingatiaji wa Shirika (“CCD”) yupo kwa ajili ya kutoa usaidizi. Kama inaibuka hali ambayo haijashughulikiwa na CBC, ni wajibu kwa kila mmoja haraka kuwasiliana na msimamizi wake, piga simu ya msaada ya Alliance One kuhusu uzingatiaji (angalia “simu ya msaada kuhusu uzingatiaji” kwenye mwongozo huu), au CCD.

CBC ni msingi wa Mpango wa Uzingatiaji wa AOI na, kwa hivyo, inaongozwa na CCD na CCM. Hata hivyo, Idara ya Maadili ya Shirika mara kwa mara hushirikiana na idara nyingine, kama fedha, sheria, rasilimali watu na huduma za ukaguzi za shirika, kushughulikia maswali na hoja kwa usahihi.

Tafadhali iweke CBC katika sehemu nzuri ili uweze kuirejelea hapo baadaye. Nakala za ziada zinazweza kupatikana kwa urahisi kutoka kwenye tovuti ya AOI (www.aointl.com) au intraneti ya AOI.

Kwa sababu AOI imeunganishwa nchini Marekani, sheria za Marekani mara kwa mara zinapanuka kwenye utendaji wetu duniani kote vile vile kwenye shughuli za biashara za waajiriwa popote pale wanapoishi au kufanya kazi. Hata hivyo AOI,huendesha biashara kwenye nchi nyingi duniani na waajiriwa wetu ni raia wa nchi nyingi tofauti. Zaidi, biashara ya msingi ya Kampuni inahusisha usafirishaji wa bidhaa katika biashara ya kimataifa. Kutokana na haya, utendaji wetu unazingatia sheria za nchi nyingi, mikoa, miji na manispaa.

Kuna wakati mgogoro unaweza kuwepo kati ya sheria zinazotumika za nchi mbili au zaidi. Ukikutana na mgogoro kama huo, ni muhimu sana kuwasiliana na Afisa Mkuu wa Sheria wa Kampuni, CCD ili kufahamu namna ya kutatua mgogoro huo kwa usahihi.

**Misamaha**

Katika hali chache na sahihi, CCD inaweza kutoa msamaha wa utoaji wa CBC hii. Misamaha ya CBC kwa wakurugenzi na maafisa watendaji inaweza kufanywa na Bodi ya Wakurugenzi au Kamati ya Bodi, na itafichua mara moja inavyohitajika kwa sheria au kanuni inayotumika.

Baada ya kusoma CBC, unaweza kuwa na maswali au kukutana na hali ambayo unafikiri haijashughulikiwa vizuri. Kuuliza au kutafuta maelezo kuhusiana na sheria inayotumika au hoja kuhusu shughuli za biashara, unapaswa kuwasiliana na msimamizi wa karibu, Meneja Uzingatiaji wa Ndani, au moja kwa moja na CCD. Mwajiriwa yeyote, afisa, mkurugenzi, au wakala ameruhusiwa na kuhamasishwa kuwasiliana moja kwa moja na CCD bila umuhimu wowote wa kuuliza au kuomba ruhusa kutoka kwenye uongozi wa usimamizi.

Mkurugenzi wa Uzingatiaji wa Shirika
Alliance One International, Inc.
Simu: 919-379-4300
Email: compliance@aointl.com

Meneja wa Uzingatiaji wa Ndani ni mwajiriwa wa ndani katika kila eneo asilia ambaye anaweza kuibua hoja au maswali kuhusiana na uzingatiaji, na ni nani anaweza kukusaidia kukuelekeza kwenye rasilimali husika za kampuni, ikiwemo nyaraka ya uzingatiaji iliyotafsiriwa.

Waajiriwa wote, maafisa, wakurugenzi, na mawakala wanahitajika kutoa taarifa za uvunjwaji wa sheria au CBC ya AOI watakaoufahamu. AOI ina *Sera ya kutolipiza kisasi* ambayo inakulinda dhidi ya kulipiziwa kisasi kwa kuibua hoja kwa nia njema.

## Sheria gani inatumika?

## Alliance One International na wewe

?

*Ulifahamu?*

*Kuna mwajiriwa wa ndani ambaye anaweza kukusaidia kuibua hoja zinazohusiana na uzingatiaji na kukupatia rasilimali za uzingatiaji kwa lugha zote Kiingereza na za ndani.*

*Taarifa za mawasiliano za **Meneja wa Uzingatiaji wa ndani** zipo upande wa kushoto wa kiboksi hiki.*

## Kutolipiza kisasi

Kampuni inakutaka ufahamu kwamba, ilimradi unatenda kwa nia njema, unaweza kuibua swali au hoja yoyote juu ya suala linalohusu sheria au maadili bila kuhofia kwamba hutaaminiwa au kwamba utahatarisha ajira yako.  “Nia njema” haimaanishi kwamba unahitajika uwe sahihi – lakini inamaanisha kwamba unapaswa kusema ukweli kama unavyoelewa. Kama unahisi unahamasishwa au unasukumwa kuvunja sheria, au unashuhudia jambo lolote ambalo unafikiri linaweza kuwa ukiukwaji, lazima ulilete haraka mbele ya Kampuni. Ni ukiukwaji wa CBC kwa mkurugenzi yeyote, afisa, mwajiriwa, au wakala kulipiza kisasi au kuchukua hatua nyingine kinyume dhidi ya wale wanaotoa taarifa za ukiukwaji wa CBC kwa nia njema.  Wakurugenzi, maafisa, waajiriwa, na mawakala ambao wanalipiza kisasi dhidi ya wengine kwa kutoa taarifa za tatizo watawajibika na hatua za kinidhamu na ikijumuisha kufukuzwa kazi.  Tafadhali angalia *Sera ya Kutolipiza Kisasi* ya Kampuni na toa taarifa haraka juu ya kisasi chochote.

## Simu ya Msaada Kuhusu Masuala ya Uzingatiaji

Njia mojawapo ya kuwasilisha maswali au hoja juu ya uzingatiaji ni kwa Simu ya Msaada kuhusu Uzingatiaji ya Alliance One, ambayo inapatikana kwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki.  Simu ya Msaada ni makani sahihi ya wewe kuelezea masuala yaliyoshughulikiwa na CBC, pamoja na masuala ya fedha, udhibiti wa ndani na masuala ya ukaguzi, na hukuruhusu wewe kuibua maswali au hoja bila kujulikana ukipenda.

Unahitajika kuleta masuala ya uzingatiaji kwa Kampuni na unaweza kufanya hivyo bila ya kutaja jina lako. Hakuna kumbukumbu au kifaa chochote ambacho kinaweza kutambulisha au kuchunguza namba uliyotumia kupiga.  Unapopiga kupitia Simu ya Msaada ya Masuala ya Uzingatiaji, utaunganishwa na mtu mwengine huru ambaye ndiye anayedhibiti simu ya msaada.  Mtaalamu wa Mawasiliano ambaye anafanyakazi na kampuni hiyo, si Alliance One, atashughulikia simu yako. Katika maeneo mengi Mtaalamu wa Mawasiliano anayezungumza lugha ya ndani anapatikana.

Mtaalamu wa Mawasiliano atakusalimia na kukuuliza namna gani anaweza kukuhudumia.  Baada ya kubainisha sababu ya simu yako, taarifa zitakusanywa na Mtaalamu wa Mawasiliano kwa kuelewa kikamilifu madhumuni ya simu. Utapewa namba ya kesi na tarehe ya makubaliano ya kupiga simu tena.

Unahimizwa kutumia Simu ya Msaada kuhusu Masuala ya Uzingatiaji kueleza hoja yako au maswali. Alliance One haiwezi kufikia kiwango kikubwa cha maadili ya biashara yaliyoshughulikiwa kwenye Kanuni za Maadili ya Biashara bila msaada wako.

**Namba ya Simu ya Msaada kuhusu Uzingatiaji Kenya** inapatikana kwa kupiga simu ya jumla kwa 704 5528215.  Maelekezo ya upigaji na namba ya Simu ya Msaada ya ndani



Imebandikwa kwenye mbao zote za matangazo katika ofisi zote za Alliance One na viwanda na zinapatikana katika Kiingereza na Lugha za Ndani kwa Meneja wa uzingatiaji wa Ndani. Kwa kuongezea, Simu ya Msaada ya Masuala ya Uzingatiaji inaweza pia kupatikana kupitia Intaneti kwa aoicompliancehelpline.alertline.com

Taarifa itaandaliwa na shirika huru linalomiliki Simu za Msaada, na taarifa itapelekwa kwa CCD na CCM wa Alliance One. CCD na CCM watapitia hoja kuanza uchunguzi sahihi. Kama umetoa taarifa zako za mawasiliano, CCD wanaweza kuwasiliana na wewe kama kuna umuhimu. Kwa kesi ambayo umechagua kutokujulikana, upande wa tatu uliohuru ambao unamiliki Simu ya Msaada watajulishwa matokeo ya uchunguzi ili wakujibu pindi utakapopiga tena katika tarehe mliyokubaliana kufuatilia.

## Kufanyia kazi Kampuni Yetu

Ni sera ya Kampuni kulinda faragha ya waajiriwa wake. Kwa kuzingatia hilo:

- Unahitajika kukubaliana na sheria, taratibu na makubaliano yote ya faragha na ulinzi zinazotumika. Kwa mfano, hususan kwenye Sheria ya faragha ya Marekeni imeshughulikia ulinzi wa taarifa binafsi za matibabu, fedha, na mteja, na taarifa kuhusu watoto. Amri za Faragha za Umoja wa Ulaya zinaulinzi mkali kwa taarifa za matibabu na afya, taarifa zinazoelezea rangi au ukabila, maoni ya kisiasa, udini au imani za kifilosofia, uanachama wa chama cha biashara, au taarifa kuhusu maisha ya kimapenzi au mtu binafsi.

- Kwasababu sheria zinazohusiana na ulinzi wa faragha zina maelezo mengi na ni ngumu, lazima umwone Afisa Sheria Mkuu, CCD kabla ya kutengeneza, kusambaza, au kupitia mfumo wowote kuhifadhi data au mfumo mwingine ambao kupitia huo Kampuni inakusanya, inatumia, au kutoa taarifa zozote za mtu binafsi au taarifa kuhusu fedha, hali ya afya na matibabu, uraia au ukabila, maoni ya kisiasa, imani za kidini au filosofia, uanachama wa chama cha biashara, au maisha ya kimapenzi, au taarifa nyeti zozote zingine binafsi.

- Kama sheria ya jumla, katika kiwango ambacho Kampuni ina uwezo wa kufikia taarifa yoyote ya binafsi, ni sera ya Kampuni kutumia taarifa hizo kwa madhumuni yaliyoidhinishwa yenye kipimo, na si kuzitoa isipokuwa kwa mujibu wa sheria baada ya kushauriana na Afisa Mkuu wa Sheria au CCD. Hata hivyo, mawasiliano ya eletroniki yaliyoundwa kwa kutumia vifaa na mifumo ya Kampuni si ya faragha na AOI ina haki, kulingana na sheria inayotumika, kufikia, kupitia na kutumia mawasiliano, rekodi na taarifa zote zilizoundwa, kusambazwa na kuhifadhiwa kwa kutumia rasilimali za Kampuni. Taarifa za ziada kuhusu sera za IS za Kampuni zinapatikana kwenye Intraneti.

?

*Ulifahamu?*

***Simu ya Msaada ya Masuala ya Uadilifu*** *inaendeshwa na shirika lingine huru, na unaweza kutoa taarifa bila kujulikana, kama unapenda, au kwa simu au kwenye intaneti.*

# Faragha ya Mtu Binafsi



## Faragha ya Mtu Binafsi
(inaendelea)

- Lazima ushauriane na Afisa Mkuu wa Sheria au CCD  kabla ya kuunda sera yoyote ya faragha, iwe ni ya kutumia kuhusiana na  Intaneti au vinginevyo, na kudumisha taratibu za kutosha kuzingatia sera yoyote inayotumika.

## Mgongano wa Maslahi

Mgongano wa maslahi hutokea wakati maslahi ya mtu binafsi yanaingilia – au yana mwonekano wa  kuingiliana – na maslahi ya Kampuni nzima.  Hali ya mgogoro inaweza kuibuka wakati mkurugenzi, afisa, mwajiriwa, au wakala anachukua hatua au ana maslahi ambayo yanaweza kumkwamisha yeye kufanya kazi yake ipasavyo.  Migongano ya maslahi pia inaibuka wakati mkurugenzi, afisa, mwajiriwa, wakala au mmoja wa familia yake, anapokea mafao binafsi yasiyosahihi kama matokeo ya nafasi yake na Kampuni.  Uuzaji Hisa,  Fursa za Ushirika na, Maslahi na Uwekezaji wa Biashara ni mifano ya sehemu mahususi ambazo unaweza kukumbana na migogoro ya maslahi.

Migongano ya maslahi inayoweza kutokea na miamala ya wahusuka lazima iwekwe wazi kwa njia ya maandishi kwa CCD au CLO, na kuhifadhiwa vizuri kwenye nyaraka kwa mujibu wa sera ya Kampuni. Kuwa na mgogoro si lazima kuwe kukiuka Kanuni yetu ya Maadili ya Biashara, lakini kushindwa kuyafichua.

## Uuzaji wa Hifadhi

Katika kuendesha biashara ya AOI, unaweza kumiliki nyaraka za taarifa kuhusu Kampuni au vitu vingine ambavyo havipatikani kwa umma. (“taarifa zisizo za umma”).  Lazima udumishe usiri wa taarifa ambazo si za umma na huwezi kuzitumia pamoja na manunuzi na mauzo ya hifadhi ya kampuni au kitu kingine ambacho kinahusiana na taarifa, au kuitumia kumdokeza mtu mwingine kuhusu taarifa.

Sheria za nchi nyingi, hasa Marekani, zinakuzuia kununua au kuuza akiba ya kampuni au hifadhi nyingine wakati unamiliki taarifa ambazo si za umma. Chini ya Sera ya Kampuni na Sheria za Marekani, taarifa ni kitu kama:

- Kuna uwezekano mkubwa kwamba mwekezaji atazingatia taarifa za muhimu katika kubaini iwapo kufanya biashara katika hifadhi; au
- Taarifa, kama ikifanywa kuwa ya umma, inaonekana kuathiri bei ya soko la hifadhi ya kampuni.

Taarifa zinaweza kuwa kitu hata kama zinahusiana na matukio ya hapo mbeleni, na kama ni muhimu tu pale zinapochukuliwa pamoja na taarifa za umma zilizopo. Nyaraka za taarifa zinaweza kuwa nzuri au mbaya. Taarifa ambazo si za umma zinaweza kuwa nyaraka hata kwa kuzingatia



kampuni ambazo haziuzi akiba kwa umma, kama zile  zenye dhamana kubwa au mikopo ya benki. Kwa hivyo, inategemea na ukweli na hali, taarifa ambazo zinaweza kuchukuliwa kama nyaraka zinajumuisha, lakini si ukomo:

uwezekano au halisi

- Matangazo ya kipato au makadirio, au mabadiliko ya tangazo lililopita au makadirio;
- Matokeo ya fedha;
- Kupungua na kuongezeka kwa akiba kwa ajili madeni mabaya;
- Kuongezeka au upunguaji wa utendaji;
- Bidhaa mpya, utengenezaji au ugunduzi;
- Kesi kubwa au vitendo vya serikali;
- Muunganiko, upatikanaji, ofa za zabuni, biashara za pamoja au mabadiliko katika samani;
- Mabadiliko ya mapendekezo ya mchambuzi au viwango vya deni;
- Matukio hukusiana na hifadhi ya Kampuni (mf. Makosa kwenye hifadhi kubwa, kuitwa kwa hifadhi kwaa jili ya kuokoa, mipango ya kuuza tena, ufunguaji wa hisa, mabadiliko katika malipo, mabadiliko ya haki ya wadau wa hifadhi au wauzaji wa umma au binafsi wa hifadhi ya ziada);
- Mabadiliko katika udhibiti wa Kampuni au maendeleo yasiyo ya kawaida ya utawala;
- Ukopaji usio wa kawaida;
- Matatizo ya ukwasi; na
- Mabadiliko katika wakaguzi au taarifa za mkaguzi kwamba Kampuni haitegemei taarifa ya ukaguzi.

Usifanye biashara kwenye akiba za Kampuni au hifadhi nyingine wakati unamiliki nyaraka za taarifa ambazo si za umma. Vizuizi vinajumuisha biashara katika Mpango wa 401(k) wa Kampuni, kama vile uchaguzi wa kuelekeza tena michango ya baadaye au kupanga tena salio la akaunti zilizopo ambalo limetokana na mauzo au manunuzi (kitaifa au vinginevyo) ya akiba ya AOI.  Kuongezea, uchaguzi wa akiba iliyopo unakatazwa kama unafanyika wakati unamiliki nyaraka za taarifa zisizokuwa na umma.

Kama nyaraka za taarifa zisizo za umma zinahusisha kampuni nyingine (katika hali ya umoja, kwa mfano), unazuiwa pia kufanya biashara kwenye akiba ya hiyo kampuni au kutoa taarifa hiyo kwa mtu ambaye anaweza kufanya biashara. Hii inatumika bila kujali iwapo mpokeaji wa taarifa anahusiana na ndani au ni mtu umoja kama vile amana au ushirika, na bila kujali iwapo unapokea mafao ya pesa yoyote kutoka

?

## *Ulifahamu?*

*Katika shughuli zako za kawaida unaweza kukutana na taarifa ambazo huruhusiwi kuzitumia kuamua iwapo kununua au kuuza akiba ya Kampuni. Kujifunza zaidi kuhusu "biashara ya ndani" rejea Sera ya Kampuni ya Biashara ya Ndani, ambayoinaweza kupatikana kwenye ukurasa wa intaneti wa uadilifu.*



## Uuzaji wa Hifadhi
(inaendelea)

kwa mpokeaji. Mtu yeyote anayekiuka sheria hii atawajibishwa kwa ulafi, adhabu ya fedha, na kufungwa jela.

Taarifa zitachukuliwa kama za "umma" katika siku ya tatu ya biashara baada ya taarifa hizo kutangazwa kwa umma na afisa mahususi wa Kampuni. AOI, wakurugenzi wake, maafisa, waajiriwa, na mawakala wanaweza kuwajibishwa kwa kosa la jinai au madai kwa kukiuka sheria ya hifadhi. Maafisa, waajiriwa na mawakala ambao wanakiuka sera hii wanawajibishwa kwa kuadhibiwa, hadi kusitishwa kwa ajira zao. Vile vile kujiuzulu kwa mkurugenzi kunaweza kufikiriwa.

Kwa meongozo zaidi, tafadhali rejea kwenye Bny's *Sera ya Biashara ndani ya Kampuni*, au wasiliana na Ofisa Mkuu wa Sheria wa Kampuni.

## Fursa za Shirika

Wakurugenzi, maafisa, waajiriwa, na mawakala wanazuiwa kujichukulia wenyewe, au kuwapa wengine fursa ambazo zimegunduliwa kwa kupitia mali za shirika, taarifa au nafasi bila idhini ya Bodi ya Wakurugenzi. Hakuna mkurugenzi, ofisa, mwajiriwa, au wakala anayeweza kutumia mali, taarifa au nafasi ya shirika kwa manufaa bianfsi isivyo halali, wala kushindana na Kampuni moja kwa moja na si moja kwa moja. Wakurugenzi, maafisa, waajiriwa na mawakala wanawajibika kwa Kampuni kuongeza maslahi yake kisheria pindi fursa ya kufanya hivyo inapotokea. Wasiliana na CCD kwa mwongozo kuhusu mgongano wowote wa maslahi.

## Hongo na Rushwa

Rushwa ni kinyume cha sheria, rushwa iwe inatolewa kwa wafanyakazi wa serikali (rushwa ya sekta za umma), au kampuni au raia binafsi (rushwa ya sekta binafsi). Inadhuru jamii ambako tunafanya kazi. Lazima tushiriki katika juhudi za kuondoa rushwa.

Kila mmoja wetu lazima afuate kikamilifu sheria zote za dani na nje za kupinga rushwa. Sheria za nje za kupinga rushwa ni sheria za nchi mmoja ambazo zinapinga rushwa kwenye nchi nyingine.

Kamwe tusitoe rushwa kwa namna yoyote, pamoja na:

- Malipo ya "bahashishi" – hata kama ni kiasi kidogo.
- Malipo ya kupata idhini isivyo halali, kodi za upendeleo au huduma kwa wateja, leseni, vibali aumafao yoyote mengine.
- Malipo kwa wapinzani kwa wapinzani kubadilisha na taarifa za siri.
- Malipo ya kazi yasiyo ya kawaida yanayofanywa au kudaiwa kwa nia ya rushwa.
- Motisha za mteja zisizo sahihi.
- Malipo ya kupata masharti ya kupendeleo kutoka kwa watoa mikopo, kama vile benki.



Ingawa rushwa ni kinyume cha sheria na sera ya Kampuni bila kujali iwapo rushwa inatolewa kwa afisa wa sheriakali au raia, mteja au msambazaji, masuala ya pekee yapo kwa kila tukio ambalo waajiriwa wa Alliance One wanatakiwa kufahamu.

*Masuala ya Rushwa kwenye Sekta za Umma*

Sheria ya Rushwa ya Nje nchini Marekani ("FCPA") imefanya kuwa kinyume cha sheria kwa kampuni ya Marekani, kama vile AOl, au matawi yake mengine ulimwenguni, wabia, mawakala, wauzaji wawakilishi au washauri na waajiriwa wa vitengo vyote hivi, kumpa, kutoa au kuahidi kitu chochote cha thamani kwa mfanyakazi wa serikali kwa matarajio, matumaini au nia kwamba mfanyakazi huyo atashawishi maamuzi ya kufanya biashara na Kampuni.  Hii inajumuisha kupata biashara mpya, kuendelea na biashara ya sasa, au kupata manufaa kadhaa.

FCPA inatekelezwa kijinai na Idara ya Sheria ya Marekani ("DOJ") na kimadai na Tume ya Hifadhi na Biashara ("SEC").  FCPA sehemu kuu mbili: (a) Vifungu vya kupiga hongo (b) na vifungu vya hesabu.

(a) Vifungu vya kupinga hongo vya FCPA vinafanya kuwa jinai malipo yasiyo halali kwa maafisa wa serikali. Mambo ya msingi ya vipengele vya kupinga hongo vya FCPA ni:

- Malipo, ofa, au ahadi ya kitu **chochote cha thamani**;
- kwa mfanyakazi **yeyote wa serikali**, chama chochote cha siasa cha Marekani au wafanyakazi wa cham, mgombea wowote wowote kwa ajili ya ofisi ya kigeni ya chama au mtu mwingine yeyote huku akijua kwamba kiasii chochote cha malipo au ahadi ya kulipa itatolewa kwa mmoja wa watu hao;
- kwa nia mbaya ya kutoa **rushwa** ili **kushawishi maamuzi ya mfanyakazi wa serikali,** kumkumbusha mtu huyo kufanya au kutokufanya kitendo chochote katika kukiuka wajibu wake kisheria, au  kumkumbusha mtu huyo kutumia ushawishi wake na serikali za kigeni kuathiri au kushawishi kitendo chochote cha serikali au maamuzi;
- kusaidia katika **kupata au kudumisha biashara, na** au kuelekeza biashara kwa, mtu au kampuni yoyote.

?

*Ulifahamu?*

*Sera ya Kmapuni inazuia aina yoyote ya hongo, bila kujali iwapo mtu anayepokea hongo ni afisa wa serikali au raia binafsi.*



# Hongo na Rushwa
(inaendelea)

?

*Ulifahamu?*

*Kwa kuongezea kwenye hongo kuwa kinyume cha sheria, pia ni kosa kubwa la tofauti kupotosha uendeshaji wa biashara kwenye vitabu vya Kampuni na kumbukumbu.*



“Kitu chochote cha thamani” kinaelezea kiujumla. Ikijumuishwa pesa taslimu, pia inajumuisha aina yoyote ya faida kwa familia na hata uwezo wa kuelekeza faida kwa mtu mwingine. Mifano inajumuisha:

- Fedha taslimu, zinazolingana na fedha, au mafao mengine (ukaguzi wa wasafiri, mafao ya kusafiri);
- Huduma za mtu binafsi;
- Ajira au ofa ya ajira;
- Michango ya kujitolea kwa faida ya mfanyakazi;
- Michango ya kisiasa; na
- Matumizi mengine ya mali za Kampuni (pamoja na lakini si ukomo na ndege, nyumba, magari, majahazi, n.k.) na maafisa wa serikali au wafanyakazi wao badala ya lengo la kutangaza, kuonyesha au kuelezea bidhaa au huduma za Kampuni.

(b) Utoaji wa hesabu wa FCPA unahitaji kampuni kuhifadhi vitabu na kumbukumbu zote zinazoonyesha kwa usahihi na usawa mwenendo wa biashara zote na kuhifadhi udhibiti wa hesabu za ndani kwa lengo hilo. Miongoni mwa mambo mengine, utoaji huu una lengo la kuzuia “fungu la fedha la kuhonga maafisa wa umma”, ufanyaji biashara bila kuingiza kwenye vitabu na mgawanyo wa matumizi yasiyo sahihi ambao unaweza kuwa njia ya kulipa hongo na kuficha mazingira ya malipo.

Ukiukwaji wa FCPA au sheria nyingine za kupinga rushwa za ndani kunaweza kupelekea kufungwa jela, faini kubwa, na adhabu nyingine. Kwa mfano, mtu anaweza kutakiwa kulipa faini ya hadi Dola za Marekani 250,000 au/na kufungwa jala kwa hadi miaka 5 kwa kila ukiukwaji wa vifungu vya kupinga rushwa; au kwa ukiukwaji wa vifungu vya hesabu, mtu anaweza kupigwa faini ya hadi Dola za Marekani milioni 5 na/au kufungwa jela kwa hadi miaka 20. Kwa kuongezea, Kampuni yenyewehukabiliwa na mashtaka, faini kubwa, na shadhabu nyingine. Mwenendo wa biashara wa ndani ambao unadharau au hata haufuati mwenendo huu si kinga. Mwajiriwa yeyote ambaye hufanya au hupanga zawadi, ofa, au ahadi ya kitu chochote cha thamani katika ukiukwaji wa sera hii anawajibishwa na Kampuni kwa kupewa adhabu kali , ikijumuisha kufukuzwa kazi.

FCPA inatumika sawa kwenye zawadi, ofa, na ahadi inayofanywa moja kwa moja na mwajiriwa au kupitia mtu fulani ambaye si mwajiriwa wa Kampuni. Kwa msingi huo FCPA hufanya kuwa kinyume cha sheria “tafuta njia nyingine” au kupuuzia ukweli au kimsingi zinapendekeza kwamba mtu mwingine anatoa zawadi, ofa, au ahadi kinyume cha sheria kwa niaba yetu. Zaidi, utoaji pesa kwa mtu mwingine au kuingilia kwa imani au kwa nia kwamba mtu huyo atatoa zawadi, ofa, au ahadi isivyo halali, au kudharau kwa makusudi ukweli wa biashara ni kinyume cha sheria.

**Afisa wa Serikali ni nani?**

Kwa lengo la sera ya Kampuni, maana ya "afisa wa serikali" lazima ieleweke kuwa pana na ingejumuisha, lakini si ukomo kwa, maafisa wa forodha na uhamiaji; maafisa waliochaguliwa na kuteuliwa kama mahakimu, meya, mawaziri wa serikali na waajiriwa wengine wa serikali; maafisa au waajiriwa wa mashirika ya umma ya kimataifa kama vile Umoja wa Mataifa, Benki ya Dunia au Mfuko wa Fedha wa Kimataifa; wasimamizi wa viwanda mbalimbali vya tumbaku kama vile wakaguzi wa kilimo, maafisa wa vyama vya siasa au wagombea kwa ajili ya ofisi za siasa.

**Ya muhimu sana, waajiriwa wote wa ngazi au nafasi yoyote ya wanaohodhi tumabaku inayomilikiwa au kusimamiwa na serikali,ni maafisa wa serikali.** Hiyo inajumuisha wateja wa Kampuni, pamoja na lakini si ukomo:

- Global TobaCCD Ltd.
- Imperial VinaDanang
- Japan TobaCCD, Inc.
- Khanh Hoi Cigarette Factory
- Tian Li International Co. Ltd.
- Vietnam National TobaCCD Corporation
- FabrikaDunhana Sarajevo, Bosnia & Herzegovina
- SocieteNationale des Tabacs et Allumettes
- China TobaCCD International Inc.
- Eastern Company S.A.E.
- National TobaCCD Enterprise
- Sekap, S.A.
- Korea Tomorrow and Global Corp.
- Iran TobaCCD Company
- RegieLibanaise des Tabacs et Tombacs
- Libyan TobaCCD Company LTC
- Taiwan TobaCCD & Liquor Corporation
- Thailand TobaCCD Monopoly
- Regie National des Tabacs et des Alumettes
- Manufacture des Tabacs de Kairouan
- Vietnam TobaCCD Import & Export Co
- National Cigarette and Match Industries Ltd.
- Saigon TobaCCD Company
- Thang Long TobaCCD Company
- Saigon Industry Corporation
- Khatoco

Hii inamaana gani? Inamaana kwamba mtu yetote anayefanyakazi kwa ajili ya serikali, kuanzia Waziri Mkuu hadi mpeleka barua wa posta, anachukuliwa kama "afisa wa serikali" kwa lengo la sera za Kampuni. Mwajiriwa yeyote wa mahakama, pamoja na jaji, makarani, n.k., wote ni "maafisa wa serikali" chini ya sera hizi. "Maafisa wa sherikali" wanaweza pia kujumuisha wajumbe wa familia za maafisa wa serikali au watu waliochaguliwa na maafisa wa serikali kupokea kitu fulani cha thamani kama kitu cha thamani kinachotolewa kwa mjumbe wa familia ni kweli njia ya kupata faida kutoka kwa afisa wa serikali.

?

*Ulifahamu?*

*Baadhi ya wateja wetu wanachukuliwa kama maofisa wa serikalii chini ya sheria za kupinga rushwa. Rejea kwenye orodha katika upande wa kushoto kuona mifano ya wateja hao, na mjulishe CCD au CCM kama unaamini mteja ambaye unazungumza naye anamilikiwa au kuendeshwa na serikali, na hayuko kwenye orodha hii.*



Kama una maswali kuhusu iwapo mtu anaehusika katika biashara amejumuishwa kwenye sheria husika ya kupinga rushwa, unatakiwa kumwona CCD.

### Kwa taarifa zaidi

*Ingawa kipengele hiki inashughulika na lipaji wa safari na burusani kwa maofisa wa serikali, Sera ya Kampuni ya safari na burudani ulimwenguni pia inaelezea gharama gani unaweza kuingia kwa ajili ya safari yako binfsi na burudani kwa ajili ya mwaajiriwa.*

**Ulipaji wa Zawadi, Safari na Viburudisho kwa Maafisa wa Serikali**

FCPA inakataza utoaji "kitu chochote cha thamani" kwa maafisa wa kigeni, isipokuwa katika mwongozo finyu.

**Zawadi:** unaweza kutotoa zawadi kwa ofisa wa serikali kwa matarajio kwamba ofa au zawadi itaipatia Kampuni manufaa ya kiupinzani. Zawadi yoyote kwa afisa wa serikali lazima kabisa ikubaliane na Sera hii. Kama suala la jumla kanuni zifuatazo zinatumika: (i) zawadi ya fedha taslimu kwa maafisa wa serikali kamwe hairuhusiwi; (ii) zawadi ndogo inayobeba nembo ya Kampuni inaweza kutolewa kwa afisa wa serikali kama ishara ya heshima au nidhamu au fadhila kwa ajili ya wema; (iii) zawadi lazima iwe na thamani ya kawaida, kawaida kwa nchi inayohusika na inaendana na tukio; na (iv) zawadi lazima iruhusiwe chini ya sheria za ndani na mwongozo wa wakala wa serikali anayehusika. Lazima upate idhini ya maandishi kutoka kwa CCD wa kampuni kabla ya kutoa zawadi kwa ofisa wa serikali, pamoja na waajiriwa wa wateja wa Kampuni inayohodhi. Zawadi lazima iwe imegharamiwa au elezewa vizuri kwenye uzingatiaji na *Sera ya Dunia ya Gharama za Zawadi*.

**Gharama za Safari:** kwa ujumla, maswali kuhusiana na safari na burudani vinashughulikiwa na Sera *ya kampuni ya Safari na Burudani.* Hata hivyo, malipo kwa kampuni kwa ajili ya safari, malazi, pesa ya kujikimu kwa maafisa wa serikali (ikijumuisha wateja wetu tunaohodhi) lazima yaidhinishwe mapema na CCD . Kama suala la jumla, kanuni zifuatazo zitatumika: (i) gharama zinazohusiana moja kwa moja na utangazaji au uwezeshaji wa biashara ya Kampuni tu itarejeshwa; (ii) nauli ya ndege ya kawaida tu (si kiwango cha juu) itarejeshwa; (iii) Kampuni haiwezi kuchagua maafisa mahususi wa serikali ambao watasafiri (kwa usahihi zaidi, wakala wa serikali au mteja wa AOI lazima afanye hivyo); na (iv) safari za maafisa waliochaguliwa tu ndiyo zitalipwa, si gharama zinazoletwa na wajumbe wa familia za maafisa.

**Burudani za Biashara:** Huwezi kuburudisha maafisa wa serikali kwa matarajio kwamba burudani hiyo (au ofa ya burudani) itaipa kampuni faida ya kiushindani. Tabia njema ya Biashara au burudani ambayo inaweza kuwa sahihi unaposhughulika na wateja ambao hatuwahodhi haiwezi kuwa sahihi unaposhughulika na wateja ambao tunahodhi (maafisa wa serikali). Burudani kwa Maofisa wa serikali inaruhusiwa



pale ambapo tu gharama  (i) moja kwa moja zinahusiana na utangazaji, uonyeshaji au uelezaji wa biashara ya kampuni; (ii) kiwango cha kawaida,kwa tukio na inachukuliwa katika kipindi fulani wakati; (iii) imeruhisiwa chini ya sheria ya ndani na mwongozo wa waajiriwa wa kiofisi; (iv) inaendana na tamaduni za ndani; na (v) huepuka mwonekano wa kutokuwa sahihi kama una mashaka yoyote kuhusu iwapo gharama za burudani yoyote si sahihi lazima uwasiliane na CCD wa kampuni.

Lazima uhakikishe kwamba zawadi yoyote, safari au birudani inayotolewa kwa maafisa wa serikali inaendana kikamilifu na sera za Kampuni, bila kujali tamaduni au taratibu za ndani.

**Malipo ya Uwezeshaji au "rushwa"**:  Katika baadhi ya nchi, waajiriwa wa serikali wanaomba malipo kiasi kuharakisha au kuwezesha vitendo vya kila siku vya serikali. Malipo hayo yanaruhusiwa tu katika hali zifuatazo:

- Malipo ni kidogo;
- Malipo ni kwa ajili ya kupata hatua ya kiserikali ya kawaida na kampuni vinginevyo imekamilisha mahitaji yote kwa ajili ya hatua ya serikali. Hatua ya kila siku ya kiserikali haijumuishi maamuzi ya wazi kuhusiana na biashara
- Malipo si sehemu ya mfululizo wa malipo kama hayo; na
- Malip yanategemeana na sheria za ndani, taratibu, na masharti, au hakuna njia nyingine ya kuwezesha hatua ya kila siku ya kiserikali.

La muhimu sana,  ingawa malipo haya katika matukio  machache sana yanaweza kuruhusiwa chini ya FCPA, hayawezi kuruhusiwa chini ya sheria za nchi nyingine, ikiwa ni pamoja na nchi ambako malipo yanahitajika, Sheria ya Rushwa ya UK, Mkataba wa kupinga rushwa wa O.E.C.D. na nyinginezo. Hivyo, malipo hayo yanapaswa kuchukuliwa, iwapo tu ni hali isiyo ya kawaida au haiepukiki. Inapowezekana, na kama una wakala mapema, kisha idhini ya maandishi inapaswa ichukuliwe kutoka kwa CCD.

Zaidi, iwapo katika matukio machache ambapo malipo hayo hayawezi kuepukwa, ni sahihi na kisheria kuhitaji malipo hayo kuelezewa kwa usahihi na kuandikwa kwa usahihi kwenye vitabu au kumbukumbu za kitengo husika cha kampuni. Si katika hali yoyote ile malipo hayo yanapaswa kufichwa kwenye vitabu vyetu na kukumbukumu. Kama una maswali kuhusiana na uwezeshaji malipo, wasiliana na CCD wa AOI.

*Kwa taarifa zaidi*

*Jifunze zaidi kuhusu uwezeshaji wa malipo na mada nyingine za uzingatiaji, tafuta mada zilizowasilishwa kwa njia ya video kwenye ukurasa wa intaneti wa uzingatiaji katika AOI.*



# Hongo na Rushwa
(inaendelea)

**Kwa taarifa zaidi**

*Kipendele hiki cha kanuni za Maadili ya Biashara, na CCD na CCM wa Kampuni ni rasilimali za kukusaidia wewe kuelewa wakati gani unafaa kutoa zawadi. Kusaidia kuelewa namna kwa ajili ya zawadi, rejea Sera ya Ulimwengu ya gharama za Zawadi.*



**Shughuli za Kisiasa na Michango**

Waajiriwa katika uwezo wao binafsi wanahamasishwa kushiriki katika taratibu za kisiasa. Lazima, hata hivyo, kwa umakini mkubwa uepuke hata kuonekana kwa kutumia hadhi ya Kampuni kumsaidia mgombea fulani au suala fulani. Katika hali yoyote ile huwezi kutumia Kichwa cha barua cha Kampuni kuunganisha na kushiriki kwako binafsi katika taratibu za kisiasa. Pia, katika hali yoyote ile Kampuni haitaweza kumrejeshea mwajiriwa pesa kwa kumchangia yeye binafsi michango ya kisiasa.

Ukiwa kama mwakilishi wa Kampuni, utashiriki tu katika ufuasi wa shughuli za kisiasa kama hasa zinavyoelekezwa na Afisa Mkuu. Kama shughuli ya kisiasa inahusisha michango ya kisiasa na au kwa niaba ya Shirika au wasaidizi wake wowote, iwe ni kwa fedha au si fedha, kisha lazima upate idhini kabla kutoka kwa CCD au CCM wa kampuni. Lazima uweke kumbukumbu za michango kwa usahihi kwenye vitabu vya Kampuni au kumbukumbu. Zaidi, lazima uwe makini usiingie kwenye shughuli ambazo zinachukuliwa kama ushawishi. Ushawishi unawajibishwa katika sheria mbalimbali za shirikisho, miji na ndani na huhusisha utoaji taarifa, na huhitaji idhini kabla kutoka kwa CCD wa Kampuni. Kama una maswali kuhusu shughuli za kisiasa, wasiliana na CCD wa Kampuni.

*Masuala ya Rushwa katika Sekta Binafsi*

**Kukubali/ Kutoa Zawadi kwa Wateja Binafsi na Wasambazaji**

AOI haitaki biashara iliyopatikana kutokana na matumizi mabaya ya heshima ya biashara. Unatakiwa kuwa makini na suala hili. Kama Mkurugenzi, afisa, mwajiriwa, au wakala, unapaswa kufanya kazi zako na majukumu yako katika namna ambayo ni kwa maslahi ya Kampuni. Hiyo inamaana lazima usiruhusu mgogoro wowote wa maslahi binafsi na uwezo wako wa kuwakilisha maslahi mazuri ya kampuni. Tumia uamuzi wako mzuri kujua ni stahifu gani ni sahihi, lakini kumbuka kanuni zifuatazo.

Katika kushughulika na wateja binafsi, unaweza kutoa au kupokea zawadi za thamani ndogo kama ishara ya heshima au urafiki. Unapaswa kufahamu thamani si tu ya zawadi binafsi, lakini pia thamani ya jumla ya zawadi anazopewa mtu au shirika kwa kipindi fulani. FEDHA TASLIMU KAMWE HAZIRUHUSIWI. Vitu vingine ambavyo haviruhusiwi ni pamoja na:

- Mikopo yoyote, isipokuwa mikopo yenye mkataba kutoka kwenye taasisi za fedha katika njia yakawaida ya biashara;
- vyakula, vinywaji,burudani, safari au malazi, au malipo kwa ajili ya vitu hivyo, isipokuwa kama mtoaji yupo na kitu kinahusiana moja kwa moja na biashara.

Si tu lazima uwe makini katika kukubali zawadi binafsi; lazima pia uwe makini kuhusu utoaji wa zawadi binafsi au faida kwa wale ambao unafanya nao biashara.

Kampuni inakutarajia kutengeneza mahusiano mazuri na wateja. Haya yanahitaji umakini binafsi na huduma. Usizoee zawadi nyingi au kutoa zawadi zenye gharama kwa wasambazaji binafsi, au watu wengine unaofanya nao biashara, na asitarajie huduma hiyo kutoka kwako. Zawadi, upendeleo na burudani vinaweza kupewa pande binafsi kama:

- zinaendana na taratibu za uendeshaji biahsara zinazokubalika;
- si za gharama na haziwezi  kuonekana kama hongo au rushwa; na
- inaendana na Kanuni hii na viwango vya kimaadili vinavyotumika.

Kwa kuwa sheria mbalimbali za kupinga rushwa zinatawala zawadi binafsi, ni muhimu kuwasiliana na CCD wa Kampuni mara zote unapotoa au kupokea zawadi.

## Michango ya misaada na Udhamini wa Ushirika

Hata inapotolewa kwa nia njema, michango ya ushirika ya msaada na ufadhili wa shirika mara nyingi umekuwa na matatizo sababu ya mahusiano muhimu kati ya mpokea msaada au ufadhili na afisa wa serikali.  Michango na ufadhili unaofanywa kwa amri ya serikali ya mteja, iwe inamilikiwa/inaendeshwa na serikali au binafsi, inaweza kuwa na matatizo pia. Kwa sababu hiyo, michango yote ya misaada ya shirika lazima iidhinishwe mapema na CCD.

## Matumizi ya Mawakala Wengine

Katika matukio fulani inaweza kuwa muhimu kuhususisha wakala mwingine kusaidia Kampuni katika kufanya biashara zake. Kampuni haitamani kujihusisha na mawakala ambao hawafanyi biashara kwa kuzingatia sheria zote na masharti, vile vile CBC yetu na sera nyingine.

**Ajira ya Nje, Maslahi na Uwekezaji wa Biashara**

Kila mara unaweza kuwa na fursa ya kufanya kazi, biashara au uwekezaji wa Kampuni. Ikiwa ndivyo, lazima ufuate miongozi ifuatayo.

Ajira ya nje au maslahi ya biashara yasiyohusiana na Kampuni, ikiwemo uwekezaji katika au huduma ukiwa mkurugenzi, afisa, mwajiriwa au mshauri wa asasi nyingine za biashara, inaruhusiwa mradi tu shughuli kama hiyo isihitilafiane au kugongana na majukumu na wajibu wa Kampuni. Ajira yoyote au uhusiano wa biashara yoyote ya nje na, au haja kubwa ya fedha kwa mshindani, shirika tanzu na mteja, muuzaji au mshindani wa Kampuni lazima ifichuliwe mara moja kwa msimamizi na CCD, na kuhifadhiwa kwenye nyaraka vizuri kulingana na sera ya Kampuni.  “Haja kubwa ya fedha” inamanisha haja yoyote ya uchumi inayoweza kushawishi au kuonekana kushawishi uamuzi wako, lakini haijumuishi kampuni, hazina za pande zote za biashara za umma, hazina za takwimu na mashirika sawa ya hisa, wakati mwekezaji binafsi hana sauti ya uwekezaji uliojumuishwa.

Unahimizwa kuhusika katika mashirika ya misaada, taaluma na raia, lakini ikiwa tu hakutahitilafiana na majukumu yako AOI. Vile vile, ikiwa unafikiria kuhusu kupata maslahi katika aina yoyote ya mali ambayo Kampuni inaweza kuwa na maslahi, lazima ufahamishe CCD.



## Matumizi ya Programu za Kompyuta

Kunakili programu za kompyuta bila ruhusa au kutumia programu zaidi ya kiwango cha leseni ni ukiukwaji wa sera ya Kampuni, na kwa matukio hayo, sheria ya hatimiliki, na inaweza kuiweka Kampuni katika ukiukwaji wa wajibu wake kwa watengenezaji wa hizo programu. Ukatazaji huu unamhusu kila mmoja bila kujali nchi, mahali na/au desturi za ndani.

## Usiri

Kila mmoja wetu ana wajibu wa kuhakikisha kwamba samani za Kampuni, zikiwa ni pamoja na taarifa za siri, zinatumika tu kwa biashara ya Kampuni. Hupaswi kutumia majengo ya AOI, mali, vifaa, mali za kiakili au huduma za mwajiriwa kwa lengo lolote ambalo halihusiani na biashara ya Kampuni bila idhini maalumu.

Samani zinajumuisha zaidi ya vifaa vinavyoonekana na miundo. Taarifa nyingi ambazo unatengeneza kama sehemu ya kazi yako ni mali --- hiyo ni, samani kubwa ya Kampuni. Taarifa hizo zinaweza kujumuisha mikakati makini, fedha, ajira, na mipang o ya biashara, na nyaraka au hifadhidata. Taarifa yoyote kuhusiana na wateja wetu, hususan taarifa yoyote iliyojumuishwa kwenye makubaliano ya usiri/kutowekwa wazi, ni sahihi na zinapaswa kuchukuliwa kama siri. Tafadhali kumbuka kwamba taarifa zetu nyingi za siri zinahifadhiwa kielektroniki.  Unapaswa kulinda data za kielektroniki kwa umakini kama ambavyo ungelinda nyaraka za karatasi.



Unapaswa kuwa makini kutoshirikisha Taarifa za siri za Kampuni na wengine, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wenzako, isipokuwa wanahitaji kufahamu kwa sababu halali za biashara. Kutoa taarifa bila idhini kunaweza kuharibu thamani yake, na kuwapa faida wengine nje ya Kampuni  isivyo halali. Pia kumbuka kwamba kutoa taarifa za siri kwa makusudi (kwa mfano, kupitia maongezi ya kizembe kwa njia ya simu ya mkononi au maneo ya umma kama ndege, lifti, maliwatoni au mikahawani) inaweza kuwa kama uharibifu kwa AOI.

Unapoondoka kwenye Kampuni, lazima usichukue taarifa zozote za siri kutoka AOI au kufichua taarifa yoyote ya siri kwa washindani, waajiriwa wapya, au mtu yeyote wa nje au shirika.

## Usahihi wa Taarifa za Fedha

Kila mmoja wetu huweka kumbukumbu au huandaa taarifa za maelezo fulani katika utekelezaji wa majukumu yake ya kazi.  Baadhi ya mifano ya kawaida ni uwekaji wazi mambo ya fedha, kumbukumbu za hesabu, mipango ya biashara, maoni yanayokubalika na taarifa za gharama. Watu wengi, ndani na nje ya Kampuni, wanategemea taarifa hizi kama za kuaminika na sahihi.  Ni wajibu wako kushikilia Sera za kampuni na taratibu na kutoa taarifa ambazo tu ni za uhakika, sahihi, zilizokamilika, zenye malengo, zinazohusiana, za wakati na zinazoeleweka.

AOI imetekeleza taratibu za kihesabu ikiwa ni pamoja na udhibiti wa ndani wa hesabu kulinda samani za Kampuni na kuhakikisha usahihi na uhakika wa  taarifa zote za fedha na zizizo za fedha. Sheria zifuatazo zinatumika kwa kila mmoja:

- Hakuna pesa, samani au matumizi ya siri ambayo hayakurekodiwa ambayo huenda yamewekwa bila sababu.
- Usishindwe kuweka kumbukumbu kwa usahihi na kuweka wazi fedha yoyote, samani, au matumizi ya Kampuni.
- Usiweke kumbukumbu za uongo kwenye vitabu vya kumbukumbu za Kampuni.
- Tusichukue hatua yoyote kuwashawishi, kulazimisha, kuhamasisha, au kupotosha isivyo halali mtu binafsi au mhasibu aliyethibitishwa kujihusisha kwenye ukaguzi wa taarifa za fedha za Kampuni.
- Usichukue malipo yoyote kwa niaba ya Kampuni ukifahamu kwamba fedha hizo huenda zikatumika kwa kitu tofauti na lengo lililoelezwa.
- Toa taarifa (katika utarabu wa kutokujulikana au siri kama ukipenda) kwa CCD, CCM, Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu, au Simu ya msaada ya masuala ya uzingatiaji suala lolote unaloweza kuwa nalo kuhusiana na mambo ya hesabu na ukaguzi.



## Usahihi wa Taarifa za Fedha
(inaendelea)

Kuhakikisha ukweli wa taarifa, ni suala la kupitiwa na wakaguzi wan je na wa ndani, pamoja na maafisa wa serikali.   Usikwepe taratibu za Kampuni na taratibu zilizoidhinishwa kwa ajili ya kukusanya na kutoa taarifa zilizo sahihi.  Wala usiruhusu msimamizi au mwajiriwa mwenzako kukuhitaji wewe kufanya hivyo.  Ukiukwaji wa utoaji taarifa za kweli unaweza kupelekea hatua za kinidhamu, ikiwemo kufukuzwa kazi. Ni jukumu la kila mwajiriwa kushirikiana na maombi ya ukaguzi.

## Mawasiliano kwa Umma

Afisa Mkuu, au wasaidizi wake, anaruhusiwa kuzungumza kwa niaba ya AOI na kupanga utolewaji wa matokeo ya fedha ya AOI. Maombi yoyote kwa ajili ya taarifa zinazohusiana na Kampuni kutoka kwa wawekezaji, wachambuzi au wadau yanapaswa kuelekezwa kwa Mhazini wa Kampuni. Maombi kutoka kwa vyombo vya habari au vyanzo vingine kuhusiana na taarifa nyingine za aina yoyote, kama vile maadili, ufanyaji kazi au majukumu ya kijamii yanapaswa kuelekezwa kwa Meneja wa Mawasiliano ya Shirika.  Kutoa taarifa za shirika kupitia njia nyingine ni ukiukwaji wa sera ya Kampuni.


## Fidia na Mafao

Mipango na sera za ulipaji wa mishahara na mafao ya Kampuni imebuniwa kufuatana na sheria zote zinazotumika na taratibu zinazoongoza masaa ya kufanya kazi, malipo ya ujira, risiti za mafao, mahitaji ya uwekaji kumbukumbu na maandishi unaohusiana.  Mahitaji haya ni magumu na yanatofautiana miongoni mwa mamlaka Nchini Marekani nan chi nyingine ambaspo kampuni inajihusisha kibiashara.Mabadiliko hayapaswi kuathiri maadili ya kampuni, kazi za kampuni, mipango na sera bila ushauri wa litaalam na Rais Masidizi wa AOI wa Rasilimali Watu.

## Kutokubagua, Fursa Sawa, & Kubughudhiwa

Kampuni inazingatia kutofanya ubaguzi na kutoa fursa sawa za ajira kwa wote.Waajiriwa wote na wote wanaoomba kazi hawata baguliwa wala kubighudhiwa kwa ukabila, rangi, dini, jinsia, utambulisho wa jinsia, kuwa au kutokuwa na ndoa, aina ya mapenzi anayopendelea, nchi anayotoka, umri, historia yake, ulemavu au uraia wake kwa kuzingatia sheria zinazotumika. Sera hii inamaanisha kutumika katika kupata wafanyakazi, uhamisho, maadili, mafunzo, utawala wa malipo na mishahara na mambo mengine yote yanayohusiana na ajira.

Kwa kuwa Serikali ya Marekani inaichukulia kampuni kama “mzabuni wa Shirikisho” kwa madhumuni mengine, Kampuni itafuata kikamilifu Fursa Sawa na Utoaji wa Pamoja wa zanuni za serikali.



Kumbughudhi au kufanya ubaguzi kwa wafanyakazi wenzako haikubaliki.  Tunategemea hivyo hivyo kutoka kwa wageni wote kama vile wateja na wasambazaji waliopo na watakaokuwa wateja na wasambazaji wetu.

Bugudha ya kingono imezuiwa kabisa na haita vumilika hata kidogo. Bugudha hii inajumuisha aina yeyote kiasilia, kimwili, kwa maneno ikiwa ni pamoja na kupandishwa cheo, kupendelewa kwenye kazi, au namna nyingine itakayotokana na kuhusishwa kwa ngono kutakakoleta mazingira ya kazi kuwa mabaya.

Wafanyakazi watafuata sheria zote za kazi na kanuni za ajira zinazoongoza unyanyasaji kazini. Mfanyakazi atakayejihusisha na unyanyasaji au bugudha atashughulikiwa ipasavyo. Wafanyakazi wanaoamini wamenyanyaswa wafikishe malalamiko yao kwa Mwakilishi wa Rasilimali Watu na wajisikie huru kuwasiliana na Makamu wa Rais wa Rasilimali Watu wa AOI.  Unaweza pia kutoa taarifa ya unyanyasaji, iwe ni kwako binafsi au ni kwa wengine kwa njia ya Simu ya Msaada Kuhusu Masuala ya Uzingatiaji (unaweza kutojitaje wewe ni nani kama utapenda kufanya hivyo) *Sera ya Kampuni ya Kutolipiza Kisasi* hutumika kwa taarifa za ubaguzi.

?

### *Ulifahamu?*

*Kampuni ina Sera ya Kutolipoza Kisasi, ambayo inakataza aina yoyote ya kisasi dhidi ya waajiriwaambao huibua masuala kwa nia njema ua kushiriki katika uchunguzi wa makosa. Sera ya Kampuni ya Kutolipiza Kisasi inapatikana kwenye ukurasa wa intanet wa masuala ya Uadilifu.*

## Ushirikiano katika Uchunguzi wa Makosa

Ni sera ya Kampuni kushiriki kwenye uchunguzi utakaofanywa na serikali na mamlaka yake katika jambo lolote linalohusisha uvunjwaji wa sheria au kughushi. Uchunguzi ni suala la kisheria na unahitaji kuhusisha ushauri wa kisheria. Huruhusiwi kujihusisha na mazungumzo yeyote ya kisheria hadi Mshauri wa Kisheria wa Kampuni awepo. Hakikisha afisa wa sheria anajitambulisha kwako na usitoe taarifa zozote za kampuni kama afisa huyo hana kibali cha mahakama kinachoruhusu kufanya hivyo.  Maafisa wa serikali pekee ndio wenye haki ya kuweza kusoma au kupata taarifa chini ya mamlaka ya amri ya mahakama (yaani kwa kibali cha upekuzi).  Iwapo serikali itahitaji taarifa hizo, kampuni ina haki ya kudurufu chochote kitakachochukuliwa. Hata katika hatua hii, lazima ufanye jitihada zinazowezekana kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Kampuni au CCD.

Afisa yeyote anayesimamia sheria au mwakilishi mwengine wa serikali anayehitaji taarifa za kampuni anapaswa ajulishwe kwamba Kampuni itatoa ushirikiano lakini tu baada ya kumfahamisha Mwanasheria Mkuu wa Kampuni au CCD ili waweze kutoa mwongozo wa namna ya kujibu.



## Ushirikiano katika Uchunguzi wa Makosa
(inaendelea)

Zaidi ya uchunguzi wa serikali, Idara ya uzingatiaji ya Kampuni inaweza kufanya uchunguzi wake binafsi.  Waajiriwa wote wanategemewa kutoa ushirikiano kikamilifu pale kampuni itakapofanya uchunguzi wa ndani. Kwa maelezo zaidi, rejea Sera ya Uchunguzi wa Ndani Ulimwenguni. Hakuna mkurugenzi, afisa, mwajiriwa au wakala atakayemshambulia mtu yeyote atakayetoa taarifa za kweli kwa afisa anayesimamia sheria kuhusu hali ya kutaka kuvunjwa au kuvunja sheria. Zaidi ya hayo, ni kwenda kinyume na Sera ya Kampuni ya Kutolipiza kisasi pale mwajiriwa atalipiziwa kisasi kwa kutoa taarifa za ukweli kuhusu masuala ya kisheria au kimaadili.

## Utunzaji Taarifa

Kampuni inatumia Program ya Utunzaji Taarifa ili kuwa na mfumo bora wa kutunza, kulinda na mwishowe kutupa taarifa za Kampuni.Taarifa za Kampuni zitatunzwa ili kuwiana na matakwa ya kisheria, kufikia mahitaji ya kibiashara au ya kisheria ya Kampuni au kuhifadhi taarifa kama inavyotakiwa na sheria kwa sababu ya kuhusiana uhitaji unaoweza kujitokeza au uliopo mahakamani, uchunguzi wa kiserikali, kuitwa mahakamani, madai, au mchakato unaofanana  zitakazozuia kwa muda utupaji wa taarifa husika.Kwa maelekezo zaidi, na kuhusu Ratiba ya Utunzaji wa Taarifa, rejea Sera ya Utunzaji wa Taarifa au wasiliana na Afisa Mkuu wa Sheria.

# Ufanyaji Kazi katika Mazingira Yetu

## Mahali pa Kazi Bila Madawa

Kampuni imejizatiti kuhakikisha kwamba waajiriwa wote wanajitenga na kutojihusisha na dawa za kulevya kinyume na sheria mahali pa kazi. Shughuli hizi kinyume na sheria ni pamoja na utumiaji wa dawa za kulevya na matumizi mabaya ya dawa za binadamu zilizoruhusiwa. Kufanikisha lengo hili, kampuni imeanzisha Programu ya Uhamasishaji Kuhusu dawa.

Kampuni imeridhia Sheria ya Kutokuwa na dawa Mahali pa Kazi ya 1988 (DFWA) inayoitaka kampuni kuhakikisha hakuna mazingira ya utumiaji wa dawa na kusimamia sheria hiyo. Sheria hii kimahususi inazuia utengenezaji, usambazaji, ugavi, umiliki au matumizi ya dawa mahali pa kazi. Kuifuata sheria hii ni sharti mojawapo kwenye kampuni kufanya kazi zake katika baadhi ya mikataba ya kiserikali. Kampuni itachukua hatua stahiki za kinidhamu, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi,  kwa mwajiriwa yeyote atakayekiuka sera hii. Kampuni kwa kuzingatia mazingira halisi na kwa matakwa binafsi  ya Kampuni,itamuhitaji mwajiriwa husika kuingizwa kwenye program ya usaidizi wa kuachana na dawa**.**



Kila mwajiriwa ana wajibu wa kukubali kumshauri mwakilishi wa rasilimali watu au Makamu wa Rais wa Rasilimali Watu wa AOI ndani ya siku tano kuhusu chochote anachohisi kuhusu matumizi ya dawa binafsi au waajiriwa wengine inapotokea mahali pa kazi. Kutotii wajibu huu wa kukubali utapelekea hatua za kinidhamu kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuachishwa ajira.

## Afya na Usalama

Afya na usalama wa mwajiriwa ni jambo nyeti sana kwenye Kampuni, na vitisho na vitendo vya dhuluma haviruhusiwi. Ni sera ya kampuni kuwa na mahali pa kazi panapofuata sheria zote za kitaifa na kimataifa na sheria ndogondogo zote zilizopitishwa kulinda afya na usalama wa waajiriwa wake.

Waajiriwa wanaokiuka sheria hizi wanadidimisha si tu afya zao, bali pia afya na usalama wa waajiriwa wengine.  Kwa sababu hii, yeyote yule atakayekiuka sheria hizi atachukuliwa hatua za kinidhamu na Kampuni.

**Ajira kwa Watoto, Ajira ya Lazima, na Haki Nyingine za Binadamu**

Alliance One imejitolea kupiga vita ajira kwa watoto, ajira ya lazima na dhuluma nyingine kama hizo zinapopatikana, na kutimiza hali salama na bora za kufanya kazi katika shughuli zake zote. Ahadi ya Kampuni imeakisiwa katika Kanuni yake ya Desturi za Ajira ya Kilimo na Sera ya Ajira kwa Watoto, inayoweza kupatikana kwenye intraneti, na kwenye tovuti ya Kampuni www.aointl.com.

## Mionogozo ya Mazingira

Sera ya  AOI nikufanya shughuli zake kwa kufuata sheria zilizopo kitaifa na kimataifa na sheria na miongozo ya ndani ya nchi kuhusu mazingira ili kuyalinda. Vilevile, Kampuni inajitahidi kuchukua hatua ya binafsi kuboresha masuala ya mazingira ya Kampuni. Inategemewa kuheshimu sheria zote zilizopo kuhusu mazingira na, wasiliana na CCD, kama una maswali au dukuduku kuhusu masuala ya mazingira.

## Ufanyikazi Katika Masoko

AOI inafanya biashara  duniani kote.  Mara nyingine, mambo yanayofanyika katika nchi moja yanaweza kusababisha uwazi wa kisheria wa Kampuni chini ya sheria za nchi nyingine, hasa sheria za Marekani.



## Anti-Boycott

Mgomo hutokea pale mtu mmoja, kikundi au nchi inapokataa kufanya biashara na watu au nchi nyingine. Sheria ya kuzuia mgomo ya Marekani na washirika wenzake inazuia ushiriki wa migomo kimataifa labda iwe imekubalika na serikali ya Marekani (kwa mfano vikwazo vya kiuchumi vilivyowekwa na Umoja wa Mataifa). Kampuni za Marekani na washirika wake duniani kote lazima zitoe taarifa kwa serikali ya Marekani kuhusu ombi lolote la kuhusika kwenye mgomo. Wasiliana na CCD pale utakapoulizwa kushiriki, kutimiza au kusaidia mgomo.

## Sheria za Makosa ya Jinai za Shirikisho juu ya Udanganyifu

Kama unamdanganya mtu au unamlaghai mtu mwengine au biashara kimataifa katika mikataba kuhusu masuala ya mali, unakiuka sheria kubwa sana, kama si zote, zinazotawala ambazo AOI inafanya biashara. Kwa mfano, uwasilishaji mbaya kuhusu ubora wa tumbaku, kiwango na thamani iliyofanywa kwenye ofa au nyaraka za ununuzi kwa wateja, taarifa kwa serikali au nyaraka kwa ajili ya kusafirisha au shughuli za kibenki, unaweza kuipa uhalali wa udanganyifu kwa njia ya barua au waya, ulanguzi au makosa mengine ya jinai. Vinginevyo, majadiliano kuhusu uwasilishajii huo mbaya kupitia matumizi ya simu, nakala halisi, barua za kielektroniki au posta vinaweza kuunda makosa ya jinai ya shirikisho ya udanganyifu wa barua au waya.

Sheria za Makosa ya Jinai Ya Shirikisho la Marekani juu ya udanganyifu zimepanuka, na watu binafsi wanawajibishwa kulipa faini kubwa na kufungwa kwa kukiuka sheria hizi. AOI inazuia tabia hiyo na inatarajia waajiriwa wake kufuata kikamilifu sheria zinazotumika.

## Uwajibikaji wa Raia

Kwa kuongezea katika sheria za makosa ya jinai, Kampuni inaweza kuwekwa wazi kwa uwajibikaji wa raia kwa ajili ya tabia fulani,ikijumuisha bila kikwazo kuingilia biashara na mipango ya mikataba, taarifa zisizosahihi za biashara nyingine, uainishaji wa uongo wa ubora wa bidhaa za wengine, na kashfa. Ni muhimu wakati wote kuwa wa kweli katika uainishaji wa Kampuni na kampuni na watu wengine, na kamwe usikiuke haki za wengine kwa niaba ya Kampuni.




## Utakatishaji Fedha

Ukatishaji fedha hutokea pale ambapo mtu anapojaribu kujipatia pesa kimakosa lakini huonekana halali kwa kuzisafisha kupitia biashara ambazo si za kimakosa. Sheria katika nchi nyingi zinazuia kukubali au kutumia pesa zilizopatikana kimakosa.

- Lazima ufuate sheria zote za ukatishaji fedha zinazotumika na sheria ambazo zinahitaji utoaji wa taarifa wa biashara za pesa taslimu au biashara nyingine za mashaka.

- Lazima utumie akili kupata taarifa za kutosha kuhusu wateja, wasambazaji, na wengine ambao una mahusiano nao ya kibiashara kujitosheleza kwamba pesa zao zinatoka kwenye shughuli za biashara halali.
- Lazima ufuate shera zote kuhusu mifumo ya malipo inayokubalika. Ni kinyume na sera ya Kampuni kukubali malipo ya pesa taslimu ya Ankara. Pia ni kinyume cha sera ya Kampuni, kukubali katika hali isiyo ya kawaida na kwa kibali cha CCD, kukubali malipo yanayolingana na pesa taslimu kama vile oda au uthibitisho wa wasafiri, au kukubali uthibitisho kutoka kwa mtu mwengine asiyejulikana. Kama pesa taslimu au biashara inayolingana haiepukiki, lazima uwe mwangalifu kukubaliana na maelezo na majukumu magumu ya utoaji wa taarifa kuhususiana na biashara hizo, ikijumuisha majukumu yaliyolazimishwa na Huduma za Mapato ya ndani za Umoja wa Ulaya.
- Lazima kwenye kiwango kikubwa uhakikishe wateja wote, wasambazaji, na wengine ambao unamahusiano nao ya kibiashara wako tayari kufuata kikamilifu shughuli zote za uwekaji wa kumbukumbu na wako tayari kwa usahihi kutoa taarifa za mambo yote yanayohusiana na biashara.
- Lazima uonyeshe umakini mkubwa wakati ambapo biashara inaruhusu kitu au vitu vinavyoonyesha biashara ya ukatishaji fedha kama:
    - Miongozo ya malipo isiyo ya kawadia, muundo mgumu wa mkataba usio na sababu au masharti ya malipo ya upendeleo;
    - Biashara kutoka au kwenda mahali pasipojulikana kama vivuli vya kodi au inahusiana na usafishaji fedha; na,
    - Maombi ya kutuma fedha kwa mtu asiyejulikana au akaunti isiyojulikana.

## Kupinga Dhamana na Ushindani Uliosawa



Duniani kote, shughuli za biashara za AOI lazima zifuate sheria za kupinga dhamana na ushindani uliosawa za nchi mbalimbali. Umoja wa Ulaya, msingi wa sheria ya kupinga dhamana ambao inayongoza mwenendo wa Kampuni ni Sheria ya Sherman, ambayo inatoa adhamu ya makosa ya jinai na uwajibikaji wa raia kwa kukiuka sheria za kupinga dhamana. Sheria ya Makosa ya jinai chini ya Sheria ya Sherman na sheria za kupinga dhamana zinazolingana ulimwenguni kote ni kali. Ukiukwaji wa Sheria ya Sherman ni kosa na unaweza kupelekea kufungwa kwa hadi miaka kumi na faini ya Dola za Marekani 1,000,000 kwa mtu binafsi. Kampuni inaweza kukabili faini ya hadi Dola za Marekani milioni 100 kwa ukiukwaji wa sheria hiyo.

Sheria ya kupinga dhamana zina lengo la kuhamasisha fidia. Zinazuia makubaliano au hatua za pamoja miongoni mwa washindani ambao wanaathirwa na biashara za muda au fidia. Makubaliano yafuatayo au

hatua za jumla yana athari sana kwenye fidia zinazochukuliwa kuwa kinyume cha sheria kabisa, inamaana kinyume cha sheria bila kuhusiana na athari halisi:

- Upangaji wa Bei: makubaliano kati ya washindani, upangaji au udhibiti wa bei zinazolipwa kwa wasambazaji au wanazotozwa wateja, au upangaji wa masharti au vigezo vya mauzo (kama vile masharti ya mkopo au gharama za uwasilishaji), pamoja na makubaliano na washindani kudhibiti uzalishaji katika namna ambayo itaathiri bei;
- Uaandaji mrefu: makubaliano miongoni mwa washindani kuandaa zabuni;
- Upatikanaji wa soko au wateja: uelekezaji wa bidhaa, huduma, utawala, wateja au masoko miongoni mwa washindani; au
- Migomo ya kundi: kukubaliana na washindani kuwagomea wasambazaji wa wateja fulani.

Ni muhimu kufahamu kwamba makubaliano miongoni mwa washindani ambayo yanapatikana kukiuka sheria ya kupinga dhamana hayahitajiki kuwa makubaliano ya kuwasilishwa, lakini yanaweza kuwa makubaliano yasiyozungumzwa ambayo si ya moja kwa moja kutoka kwenye ushahidi wa lazima na utendaji sambamba. Ni muhimu kufuata sheria ya kupinga dhamana ambayo inaepuka mazungumzo au mawasiliano na washindani kuhusu bei, masharti na vigezo vya mauzo, tawala, wateja, wasambazaji, viwango vya uzalishaji, au vitu vingine vya fidia ambavyo vinaweza kutumika kama ushahidi. Kuna kiwango kikubwa cha hatari chini ya sheria ya kupinga dhamana inayohusiana na mabadiliko yoyote ya taarifa za gharama au upangaji wa bei na washindani, lakini kunaweza kukawa na hali fulani ngumu ambapo mabadiliko hayo yanakubalika. Kabla ya kutoa au kubadilisha taarifa yoyote ya gharama au bei kwa au na wamshindani, lazima uwasiliane na Afisa Mkuu wa Sheria kuelezea kwa kina hali ya biashara kwa ajili ya utekelezaji huo na kupokea idhini ya Afisa Mkuu wa Sheria kabla ya kipengele au mabadiliko ya taarifa kuweza kutokea.

**Tabia ambayo inaweza Kukiuka Sheria ya Kupinga Dhamana**
Wakati shughuli kadhaa, kama zile zilizoorodheshwa hapo juu, zote ni kinyume cha sheria moja kwa moja na zinakatazwa moja kwa moja, shughuli nyingine ni kinyume cha sheria pale tu kama athari za ushindani wake zinaonekana kufunika faida ambazo zinaleta fidia. Lazima uwasiliane na Afisa wa Sheria Mkuu, CCD kabla ya kujiingiza kwenye shughuli za pamoja zifuatazo ambazo zinaweza kuibua masuala chini za kupinga dhamana:

- mikataba ya pamoja, inayotokea wakati mnunuzi anatumia uwezo wake kutangaza mauzo kwa wasambazaji wake;
- Mikataba maalum, hutokea wakati mnunuzi anapokubalii kununua mahitaji yake yote ya bidhaa fulani kwa muuzaji mmoja;



- Makubaliano yanayofunga, hutokea wakati muuzaji anapoweka masharti ya uuzaji wa bidhaa moja au huduma ambayomnunuzi ana nguvu fulani ya soko katika ununuzi wa mnunuaji wa bidhaa ya pili au huduma;
- Miungano, ufanisi, na miunganiko mingine ya biashara inayopendekezwa;
- Kukubali nafsi, au kumruhusu mwajiriwa mwengine au afisa wa Kampuni kukubali nafsi kwenye Bodi nyingine ya Wakurugenzi ya Kampuni;
- Kuwataka wateja kununua bidhaa na huduma au kutoa punguzo la bei katika kununua kiwango kikubwa cha bidhaa au huduma; na
- Utoaji wa leseni maalum au makubaliano mengine ya kiteknolojia ambayo yanazuia uhuru wa mwenye leseni au mtoa leseni.

**Ubaguzi wa Bei**

Sheria ya Ubaguzi wa Bei ya Shirikisho inafanya kuwa kinyume cha sheria kuuza bidhaa zinazofanana kwa bei tofauti kwa wakati mmoja kwa wanunuzi ambao wanashindani, kama bei inatofautiana inaumiza mteja ambaye ameonewa kuweza kushindana. Utoaji wa masharti yasiyo sawa ya ujira wa matangazo pia imekatazwa kama inaharibu uwezo wa kushindana kwa mteja anayeonewa. Utofauti wa bei unaweza kukubalika katika hali fulani kama gharama zao zinakubalika, au zinatolewa kufikia (lakini si kidogo) bei ya mshindani. Hata hivyo, kamwe usitafute kulinganisha bei na mshindani kwa lengo hili.

**Kuhodhi**

Kama uwepo wa kampuni kwenye soko una nguvu sana ambayo ina "nguvu ya soko", inamaana nguvu ya kudhibiti bei au kuondoa mashindano, mwenendo wake unaweza kufuatiliwa kwa karibu kubaini namna ilivyopata nguvu na namna inavyoitumia. Kama eneo lako lina nguvu ya soko, kama vile kwa kuwa wanunuzi au wasambazaji wa muda mrefu wa tumbaku, epuka tabia ambayo inaoenekana kuwa na lengo la kudhibiti bei au kutondoa ushindani, kama vile kuchukua hatua kwa ajili ya lengo la kumweka nje ya biashara mshindani. Wasiliana na Afisa Mkuu wa Sheria, CCD kama una maswali kuhusu kuhodhi au unahisi kwamba unaweza kuwa na nguvu ya soko.

Kuhodhi kunaweza pia kutokea wakati mashirika mawili au zaidi yanaungana pamoja kuunganisha pamoja nguvu zao za soko kudhibiti bei au kuondoa ushindani. Masuala juu ya shughuli za pamoja ambazo zinapelekea nguvu ya soko lazima ziletwe kwa Afisa Mkuu wa Sheria. CCD kabla ya kujiingiza kwenye shughuli hiyo.



# Kupinga Dhamana na Ushindani Uliosawa
(inaendelea)

?

*Ulifahamu?*

*Ingawa vyama vya biashara vinweza kuwa na msaada kwa kiasi fualni, vinawakilisha hatari ya kipekee kwasababu ya kuungana na washindani na hatari ya kutoa nje taarifa za siri ambazo zinaweza kuwa na athari mbaya mashindano kwenye soko. Inasaaidia wakati wote kuwasiliana na Afisa Mkuu wa Sheria, CCD au CCM kabla ya kujiunga kwenye vyama vya biashara*

**Vyama vya Biashara**

Shughuli za pamoja hazizuiliki kwa sababu zinafanyika kupitia vyama vya biashara. Kuwa makini wakati wowote unapojishirikisha kwenye chama cha biashara, kuwa makini zaidi na miongozo inayopangwa kabla kwa ajili ya kuzungumza na washindani. Zaidi ya hayo, usishiriki kwenye vyama vya biashara ambavyo vinakiuka sheria za kupinga ushindani, kama wajibu unaweza kupewa wajumbe bila kujali iwapo moja kwa moja wameshiriki kwenye shughuli iliyokinyume cha sheria. Kama umewahi kuhusika kwenye mkutano wa chama cha biashara ambao tabia za kupinga ushindani au kinyume cha sheria zinazungumzwa, unalazimika kuondoka mara moja na kutoa taarifa za tabia hiyo uliyoiona kwa Afisa wa Sheria Mkuu, CCD.

Wasiliana na Afisa wa Sheria Mkuu, CCD kama unashiriki kwenye chama cha biashara ambacho kinatoa programu za mabadiliko ya takwimu, ambapo data kuhusu gharama, kiwango cha uzalishaji, bei, usajili au taarifa sawa na hizo zinachapishwa kuchangia katika kuelewa uchumi wa tasnia hiyo. Programu kama hizo zinakubalika ilimradi miongozo fulani na tahadhari inafuatwa.

# Vikwazo vya Biashara

Mara chache, serikali inatekeleza vikwazo vya biashara na/au safari kuhusu kuingiza, kutoka au kusafirisha nchi za nje. Kwa mfano, vibali vya biashara Marekani kwa ujumla vinazuia Mtu yeyote wa Marekani, Mashirika ya Marekani na, wakati mwingine, wasaidizi wake wa nje, kushiriki kwenye shughuli za biashara na nchi zilizopewa vibali, ikiwa ni pamoja na kuuza biashara, au kununua bidhaa kutoka kwenye hizo nchi, kusafirisha tena bidhaa za marekani kwenye hizo nchi kutoka nchi nyingine, na kuingia mkataba na umoja wowote unaomilikiwa na serikali ya nchi iliyopewa kibali. Ni Sera ya Kampuni kufuata sheria zote ambazo zimepitishwa kuzuia kufanya biashara na nchi fulani. Tafadhali rejea kwenye *Sera ya Uzingatiaji yenye Vibali vya Biashara*, na *Muhtasari wa Vikwazo vya Biashara Marekani* kwa taarifa zaidi, na wasiliana na CCD kama una maswali au hoja kuhusiana na vibali vya biashara.

# Sheria za Usafirishaji/ Forodha

Lazima ufuate taratibu na sheria zote za usafirishaji, kama vile sheria kuhusu nyaraka mahususi za kusafirishia. hususan, waajiriwa na mawakala hawaruhusiwi kufanya malipo yasiyo maalum kwa ajili ya huduma za forodha bila idhini ya CCD.


shughuli zilizoelezewa hapo chini zinahitaji umakini wa hali ya juu:

- Umoja wa Ulaya na nchi kadhaa nyingine zina sheria zinazohitaji uwekaji wa alama kwenye bidhaa kuonyesha nchi zilikotengenezwa mnunuzi. Lazima uwe makini nazo na kuzifuata zote na sheria nyingine kuhusu uwekaji sahihi wa lebo kwenye bidhaa.
- Kampuni imepewa mamlaka ya "kufidia" uingizaji na shughuli nyingine zote zilizofanyika wakati bidhaa ilitengenezwa na kusafirishwa chini ya masharti yaliyoelezewa kwenye sheria na taratibu. Lazima uhakikishe kwamba madai ya kufidiwa hayana maelezo ya uongo.
- Usilipe au kushiriki kwenye malipo au fidia yasiyo halali.
- Usiandae au kuwezesha uandaaji wa Ankara kwa ajili ya mauzo kwa Kampuni ambayo hayalingani na bei halali ya mauzo ya bidhaa inayouzwa.
- Hati mbaya katika kuunganisha na biashara ya kusafirisha nje au barua za kusifu.
- Nyaraka zisizosahihi au zilizopotoshwa zilizoombwa na wafanyabiashara wabia.
- Ubadilishaji wa thamani haukuonyeshwa kwenye Ankara na nyaraka nyingine za kiofisi.
- Kushughulika na wabia wapya wa biashara.

?

### *Ukiukaji wa Hakimiliki Unaofaa*

*Kwa kufanya biashara ya Kampuni, unapaswa nyakati zote kutenda haki kwa huduma nyingine, na kutotumia vibaya njia isiyo ya haki kupitia matumizi mabaya, kuficha, kutumia visivyo taarifa uliyo na haki kuipata, uwasilishaji mbaya wa ukweli wa nyaraka, au desturi za ukiukaji wa haki usiofaa.*



# Sera Yetu kwa Muhtasari

AOI inakutegemea kushikilia viwango vya Kampuni vilivyowekwa hapo mwanzo kwenye Kanuni hii. Mhutasari ufuatao unaelezea namna ya kuwajibika katika mazingira ya kazi kufuatana na Kanuni.

*Fahamu na uishi kwa viwango.* Kwa kufahamu, kuelewa na kufuata sheria na sera za Kampuni zinazotumika, vile vile maadili ya msingi, kila mmoja wetu anaweza kuwa kama mfano wa kuigwa.

*Ifahamu sheria na uliza maswali magumu.* Unatarajiwa kuzifahamu sheria ambazo zinatumika mahususi kwenye kazi yako na kiwango cha uwajibikaji. Kama huna uhakika iwapo sheria au sera ya Kampuni inatumika, au iwapo ipo, uliza CCD wa Kampuni.

*Usibuni.* Usidhanie kwamba uongozi tayari unafahamu au haujali kuhusu suala au haki husika. Pia, usidhanie kwamba hakuna hatua itakayochukuliwa. Uongozi wa AOI umejitoa kuhakikisha kwamba viwango vya tabia ya maadili vinadumishwa. Tunakutaka utueleze kama kuna jambo ambalo haliko sawa.

*Usipuuze unyanyasaji, toa taarifa.* Wote tunahitaji kuchukulia sheria na sera za Kampuni kwa umakini. Kama unafikiri kwamba kuna mtu labda anavunja sheria au sera, tafadhali chukua hatua kushughulikia hali hiyo kwa kutoa taarifa kwa uongozi, CCD, Meneja wako wa Uadalifu wa ndani, Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu wa Bodi ya Wakurugenzi, au Simu ya msaada ya Uzingatiaji (bila kujulikana kama unapenda).

*Usilazimishwe.* Kamwe haikubaliki kuvunja sheria au sera, wala kamwe usijisikie kuvutiwa au kusukumwa kufanya hivyo - hata kama unafikiri uvunjwaji huo utaboresha msingi au utasaidia kufikia lengo la kiutendaji.